Dartmouth Health

| Kichwa cha Sera | Sera ya Msaada wa Fedha za Huduma za Afya | Kitambulisho cha Sera | 179 |
|---|---|---|---|
| **Maneno muhimu** | **mgonjwa, fedha, msaada, ufadhili, matibabu, hitajika, huduma, NSA, Kutojumuishwa, Yasiyojumuishwa kwenye Msaada wa Fedha, FAA** | | |

## I. Kusudi la Sera

Kubuni sera ya mpango wa utoaji wa msaada wa fedha za huduma za afya wa Dartmouth-Hitchcock Health. Sera hii inabainisha yafuatayo kuhusiana na huduma zote za dharura au huduma zingine muhimu za matibabu zinazotolewa na vituo vyote vya D-HH:

- vigezo vya kutimiza masharti ya kupokea msaada wa fedha.
- njia ambazo wagonjwa wanaweza kutuma maombi ya msaada wa fedha.
- msingi wa kutathmini kiasi cha pesa za kutozwa kwa wagonjwa wanaotimiza masharti ya kupokea msaada wa fedha chini ya sera hii na kikomo cha gharama za kutozwa kwa huduma za dharura au huduma zingine muhimu za matibabu.
- mbinu za D-HH za kutangaza sera katika jamii inayohudumiwa.

Sera hii imekusudiwa kutii masharti ya NH RSA 151:12-b, Kanuni ya Mapato ya Ndani Kifungu cha 501(r) na Sheria ya Ulinzi wa Wagonjwa na Matibabu ya Bei Nafuu ya 2010 na itasasishwa mara kwa mara kwa kiwango kinachohitajika na sheria inayotumika.

## II. Upeo wa Sera

Sera hii inatumika kwa mtoa huduma yeyote wa D-HH anayefanya kazi katika kituo chochote cha D-HH anayewajibika na kutoa huduma za dharura na huduma zingine zozote muhimu za matibabu na kutozwa na mtoa huduma wa D-HH.

Kwa makusudi ya sera hii, maombi ya "msaada wa fedha" yanahusiana na utoaji wa huduma za dharura na huduma zingine muhimu za matibabu zinazotolewa katika kituo chochote cha D-HH na mtoa huduma yeyote aliyeajiriwa na D-HH.

## III. Ufafanuzi

**Msaada wa Fedha** (unajulikana pia kama "ufadhili wa matibabu"): Utoaji wa huduma za afya bila malipo au kwa bei nafuu kwa watu wanaotimiza masharti yaliyobainishwa kwa mujibu wa sera hii.

**Familia** inafafanuliwa na U.S. Census Bureau kama kikundi cha watu wawili au zaidi wanaoishi pamoja na wenye uhusiano wa kuzaliwa, kuoana au kupangwa.

- Sheria ya jimbo kuhusu ndoa au uhusiano usio wa kindoa na mwongozo wa serikali kuu hutumiwa kubainisha anayestahili kujumuishwa katika familia.
- Kwa wanaotuma maombi wanaopata mapato kwa kutunza wazee wenye ulemavu nyumbani kwao, mzee huyo mwenye ulemavu atahesabiwa kama

mwanafamilia na mapato yake yatajumuishwa katika mchakato wa ubainishaji.

- Kanuni za Huduma ya Mapato ya Ndani ambazo zinafafanua anayeweza kubainishwa kama mtu anayetegemea msaada wa wengine kwa makusudi ya ushuru, hutumiwa kama mwongozo wa kuthibitisha ukubwa wa familia katika utoaji wa msaada wa fedha.

**Msaada wa Fedha kwa Msingi wa Kukisia:** Utoaji wa msaada wa fedha za huduma muhimu za matibabu kwa wagonjwa ambao hawana Fomu ya Msaada wa Fedha ya D-HH iliyojazwa kwa sababu ya ukosefu wa hati zinazohitajika au kutopokea mawasiliano kutoka kwa mgonjwa. Ubainishaji wa hali ya kutimiza masharti ya kupokea msaada unalingana na hali za maisha ya mtu zinazoonyesha mahitaji ya fedha. Msaada wa fedha wa muda haupatikani kwa ajili ya kulipa madeni ambayo hayakushughulikiwa na bima ya Medicare.

**Familia:** Kikundi cha watu ambao kimsingi wanaishi katika nyumba moja walio na uhusiano unaotambuliwa kisheria (damu, ndoa, kupangwa), pamoja na wazazi ambao hawajaoana wanaotunza mtoto au watoto pamoja. Familia ya mgonjwa inajumuisha mgonjwa, mchumba, mtoto asiyejitegemea, wachumba ambao hawajaoana waliopata mtoto pamoja anayeishi nao katika nyumba moja, wachumba wa jinsia moja (waliooana au walio na uhusiano usio wa kindoa) na wazazi waliotajwa kwenye hati ya malipo ya ushuru ya mtoto ambaye ni mtu mzima.

**Mapato ya Familia:** Jinsi ilivyofafanuliwa chini ya mwongozo wa kiwango cha umaskini (FPL) wa serikali kuu kama inavyochapishwa kila mwaka na U.S. Department of Health and Human Services kulingana na:

- mishahara, malipo ya kutoajiriwa, Fidia ya Wafanyakazi, Ustawi wa Jamii, Mapato ya Ulinzi wa Ziada, msaada wa umma, malipo ya wanajeshi waliostaafu, manufaa ya waathiriwa, malipo ya uzeeni au mapato ya kustaafu, riba, migawo ya faida, kodi za nyumba, mirabaha, mapato ya mali, amana, msaada wa elimu, masurufu, fedha za malezi ya mtoto, msaada kutoka nje ya familia na vyanzo vingine mbalimbali vya mapato;
- manufaa yasiyo ya pesa taslimu (kama vile vocha za chakula na ufadhili wa nyumba) **hayahesabiwi**;
- mapato ya kabla ya kutozwa ushuru;
- mapato ya wanafamilia wote (Wasio jamaa, kama vile watu wanaoshiriki nyumba, **hayahesabiwi**).

**Mgonjwa asiye na bima ya afya:** Mgonjwa asiye na bima au chanzo kingine cha malipo ya matibabu yake.

**Mgonjwa mwenye bima isiyotoa msaada wa kutosha:** Mgonjwa aliye na bima au chanzo kingine cha malipo, ambaye gharama anazolipia mwenyewe zinazidi uwezo wake wa kulipa kama inavyobainishwa kulingana na sera hii.

**Gharama za Jumla:** Gharama za jumla za huduma za afya za mgonjwa kulingana na viwango kamili vilivyobainishwa na shirika.

**Hali za matibabu ya dharura:** Kama inavyofafanuliwa ndani ya maana ya kifungu cha 1867 cha Sheria ya Ustawi wa Jamii (42 U.S.C. 1395dd), hali ya matibabu inayoashiriwa na dalili kali za ghafla (ikiwa ni pamoja na maumivu makali) ambapo matibabu ya haraka yasipopatikana, huenda ikasababisha:

- hatari kubwa kwa afya ya mtu (au, kwa kuzingatia mwanamke mjamzito, afya ya

mama au mtoto wake aliye tumboni

- madhara makubwa ya utendakazi wa mwili
- kutofanya kazi ipasavyo kwa sehemu au ogani fulani ya mwili kwa kiwango kikubwa
- kwa kuzingatia mwanamke mjamzito:
    - muda ambao hautoshi kuwezesha kuhamishwa kwa usalama hadi kwenye hospitali nyingine kabla ya kujifungua.
    - hatari kwa afya au usalama wa mama au mtoto aliye tumboni iwapo atahamishwa au kuruhusiwa kuondoka hospitalini.

**Huduma Muhimu za Matibabu:** Kama inavyofafanuliwa na bima ya Medicare kwa kuzingatia vipengee au huduma za afya, ni huduma muhimu na zinazohitajika za uchunguzi na matibabu ya ugonjwa au jeraha ili kuboresha utendakazi wa sehemu au ogani ya mwili iliyoathiriwa.

**Huduma zisizo muhimu**: Vipengee au huduma za afya ambazo zinazingatiwa kuwa si huduma muhimu za matibabu.

**Huduma Zisizojumuishwa kwenye Msaada wa Fedha:** Huduma ambazo hazizingatiwi kuwa huduma muhimu za matibabu au zinazozingatiwa kuwa huduma zisizo muhimu. Sera hii inatumika kwa huduma zinazotolewa katika kituo cha D-H, APD au CMC na mtoa huduma yeyote aliyeajiriwa na D-HH. Pia, watoa huduma wanaweza kutoa huduma katika kituo cha D-H, APD au CMC kama sehemu ya huluki isiyo ya D-HH. Huduma hizi hazishughulikiwi na sera ya Msaada wa Fedha ya D-HH.

**Dartmouth-Hitchcock Health:** Kwa makusudi ya sera hii, Wanachama wa Mfumo wa Dartmouth-Hitchcock Health (D-HH) ni Alice Peck Day Memorial Hospital, Cheshire Medical Center, Mt. Ascutney Hospital and Health Center, New London Hospital na Visiting Nurse na Hospice for Vermont and New Hampshire (VNH). Hospitali zingine zote zinazopatikana New Hampshire na Vermont zinazingatiwa kuwa Si vituo Wanachama.

Sera hii inatumika katika Dartmouth-Hitchcock Clinic, Mary Hitchcock Memorial Hospital, Alice Peck Day Memorial Hospital, New London Hospital na Cheshire Medical Center.

## IV. Taarifa ya Sera

Dartmouth-Hitchcock Health (D-HH), imejitolea kutoa msaada wa kifedha kwa watu walio na mahitaji ya matibabu ya afya lakini hawana uwezo wa kifedha wa kulipia huduma hizo au gharama wanazopaswa kulipia wenyewe.

D-HH hujitahidi kuhakikisha kuwa uwezo wa kifedha wa watu wanaohitaji huduma za afya hauwazuii kutafuta au kupokea matibabu. Mgonjwa anaweza kutuma maombi ya msaada wa fedha wakati wowote kabla, wakati na baada ya kupokea huduma, ikiwa ni pamoja na baada ya akaunti yake kuripotiwa katika shirika la nje la ukusanyaji wa madeni.

D-HH itatoa huduma za matibabu ya dharura na huduma muhimu za matibabu kwa watu bila kujali uwezo wao wa kulipa au hali yao ya kutimiza masharti ya kupokea msaada wa fedha au wa serikali, na bila kujali umri, jinsia, rangi, hali ya kijamii au ya uhamiaji, mwelekeo wa kijinsia au imani ya kidini. Kwa mujibu wa Sheria ya Emergency Medical Treatment and Active Labor (EMTALA), hakuna mgonjwa anayepaswa kuulizwa maelezo ya malipo au iwapo anapokea msaada wa fedha kabla ya kupokea huduma za matibabu ya dharura.

Msaada wa fedha hauzingatiwi kuwa unachukua nafasi ya majukumu ya kibinafsi. Wagonjwa wanatarajiwa kushirikiana na utaratibu wa D-HH wa kupokea msaada wa fedha au aina zingine za malipo, na kuchangia kulipa gharama za matibabu yao kulingana na uwezo wa mtu wa kulipa. Watu wenye uwezo wa kifedha wa kununua bima za afya wanatakiwa kufanya hivyo, kama njia ya kuhakikisha kuwa wanapata huduma za afya, kwa ajili ya afya yao ya jumla na kwa ajili ya ulinzi wa mali yao ya kibinafsi.

D-HH haitaweka hatua zisizo za kawaida za ukusanyaji wa madeni kwa mgonjwa yeyote bila kwanza kujitahidi kuhakikisha iwapo mgonjwa huyo anatimiza masharti ya kupokea msaada wa kifedha. Hali zozote maalum zinapaswa kuidhinishwa na Afisa Mkuu wa Fedha. Kwa taarifa kuhusu hatua

D-H ambazo H inaweza kuchukua ili kukusanya madeni, tafadhali soma sera yetu ya mikopo na ukusanyaji. Nakala ya Sera ya Mikopo na Ukusanyaji inapatikana mtandaoni, unaweza kuomba katika Ofisi za Huduma za Fedha kwa Wagonjwa au unaweza kutumiwa kwa njia barua kwa kupiga simu kwenye 844-808-0730.

A. **Vigezo vya Kutimiza Masharti ya Msaada wa Fedha kwa Wagonjwa wa HIV.** Ili kutimiza masharti ya kupokea msaada wa fedha chini ya Sera hii, lazima mgonjwa atimize vigezo vifuatavyo:

- Awe ni mkazi wa NH au VT au mtu ambaye si mkazi anayepokea matibabu ya dharura katika kituo cha D-HH.
- Asiwe na bima au awe na bima isiyotoa msaada wa kutosha wa fedha, asiwe anatimiza masharti ya kupokea manufaa yoyote ya mpango wa afya wa serikali na asiwe na uwezo wa kulipa gharama za matibabu yake kama inavyobainishwa kwenye Sera ya Mikopo na Ukusanyaji, kulingana na mchakato wa ubainishaji wa mahitaji ya fedha chini ya Sera hii.
- Awe na Mapato ya Jumla ya Familia ya chini ya 300% ya FPL, ikijumuisha mapato ya wanafamilia wote wa mgonjwa, katika kipindi cha miezi 12 iliyopita.
- Awe na Mapato ya Jumla ya Familia yanayozidi 300% ya FPL na jumla ya madeni anayodaiwa kwa huduma alizopokea katika D-HH yanayozidi 10% ya Mapato ya Familia ya miaka 2, pamoja na 10% ya thamani ya mali za familia inayozidi kiwango cha pesa kinachoshughulikiwa na bima (kama inavyobainishwa hapa chini).
- Mpango wa HIV wa NH Cares kwa ajili ya Sehemu ya C na D. Ili kutimiza masharti ya mpango wa NH State (ufadhili wa NH Cares), lazima mgonjwa atume kwanza maombi ya bima ya NH Medicaid na anyimwe bima. Akinyimwa, na mapato yake ni chini ya 500% ya FPL, na ikiwa mgonjwa anatimiza masharti na atoe hati zinazohitajika, ufadhili utashughulikia huduma za matibabu ya HIV pekee za mgonjwa asiyelazwa. Huduma za mgonjwa anayelazwa hazishughulikiwi chini ufadhili huu, hata hivyo, gharama hizi zinahesabiwa katika gharama za kulipwa na mgonjwa mwenyewe. Utoaji wa ufadhili unahitaji kuwekwa kwa kikomo au kiwango cha juu zaidi cha gharama za kulipa kulingana na asilimia ya mapato ya mgonjwa. Gharama zinazochangia kikomo cha kuwekwa zinajumuisha gharama za matibabu ya afya, matibabu ya nyumbani, dawa, hata kama hazitolewi na watoa huduma wa D-HH. Maombi ya kupokea msaada wa fedha wa D-HH hutumwa kabla ya kuwekwa kwa kikomo cha gharama. Mali hazihesabiwi kwenye kikomo cha gharama cha Sehemu ya C na D.

  Masharti ya mpango:

- Uchunguzi wa HIV (Sehemu ya C)
- Uchunguzi wa HIV au wa mwanafamilia wa

mwanamke/mtoto aliye na HIV Masharti ya mpango wa NH State HAB (NH CARES):

- Mkazi wa NH
- Uchunguzi wa HIV
- Mapato yanayolingana na/au ya chini ya 300% ya FPL
- Lazima utume maombi ya kupata bima ya Medicaid angalau mara moja kwa mwaka

Chati iliyo hapa chini inabainisha asilimia ya gharama ambayo mgonjwa anatarajiwa kulipa mwenyewe kabla ya D-HH kuacha kukutoza gharama yoyote (malipo yanayoshirikiwa, malipo ya bima yanayoshirikiwa, malipo ya lazima au ada za ziara za kutembelea daktari) kwa huduma zozote za baadaye.

| **Mapato ya Mtu Binafsi** | **Gharama ya Juu Zaidi** |
|---|---|
| Yanayolingana au chini ya 100% ya Mwongozo wa sasa wa Umaskini wa Kitaifa | $0 |
| 101% hadi 200% ya Mwongozo wa sasa wa Umaskini wa Kitaifa | Yasiyozidi 5% ya mapato ya jumla ya mwaka (mfano: mapato ya $18,000; kikomo cha gharama cha $500) |
| 201% hadi 300% ya Mwongozo wa sasa wa Umaskini wa Kitaifa | Yasiyozidi 7% ya mapato ya jumla ya mwaka (mfano: mapato ya $33,000; $2,310) |
| Zaidi ya 300% ya Mwongozo wa sasa wa Umaskini wa Kitaifa | Yasiyozidi 10% ya mapato ya jumla ya mwaka (mfano: mapato ya $49,000; $4,900) |

- Lazima hati za malipo zitolewe na kila mgonjwa chini ya ufadhili wa Sehemu ya C au D angalau mara moja kwa mwaka, na mapato yathibitishwe baada ya kila miezi 6 ikiwa uamuzi wa D-H FAA unachukua zaidi ya miezi 6. Maelezo ya ziada yanajumuisha mojawapo ya yafuatayo:
    - Stakabadhi za hivi karibuni za malipo ya ushuru
    - Stakabadhi za hivi karibu za malipo
    - Notisi ya kuthibitisha kutoajiriwa
    - Vocha za chakula zilizokabidhiwa
    - Mapato ya ustawi wa jamii

- Inapendekezwa mgonjwa ajaze maombi maalum ya msaada wa fedha za HIV, lakini maombi ya D-HH yatakubaliwa pia. Maelezo ya ziada, kama vile makao lazima yatolewe na kufuatiliwa.

- Kwa makusudi ya kubainisha thamani ya mali, mali ni pamoja na, wala si tu: akiba, masurufu, vyeti vya amana, IRA, hisa, dhamana, 401K na fedha za uwekezaji wa pamoja. Katika kutathmini kiasi cha mali kwa makusudi ya kuthibitisha iwapo mgonjwa anatimiza masharti ya kupokea ufadhili wa hapo juu:

    - Fedha za akiba (ambazo zinajumuisha akaunti za akiba, masurufu au vyeti vya amana) hulipwa hadi 100% ya FPL.
    - Akaunti za fedha za kustaafu (ambazo zinajumuisha IRA, hisa, dhamana, 401K na fedha za uwekezaji wa pamoja) hulipwa hadi kiasi cha $100,000, hisa zisizo na riba ya kudumu katika makazi ya msingi hulipwa hadi kiasi cha $200,000 kwa wanaotuma maombi wenye umri wa hadi miaka 54, na hisa zisizo na riba ya kudumu katika makazi ya msingi hulipwa hadi kiasi cha $250,000 kwa wanaotuma maombi wenye umri wa miaka 55 au zaidi.
    - Migawo ya faida inapotajwa kwenye malipo ya ushuru, vyanzo vya migawo hiyo ya faida vitahitajika pamoja na taarifa ya bei ya hivi karibuni ya sokoni.
    - Hati za fedha zote za malipo ya amana na uwezo wa kufikia fedha hizo zitahitajika.
- Tii masharti ya kutuma maombi ya mpango wa bima ya afya iliyoidhinishwa ya Mpango wa New Hampshire au Vermont Healthcare Exchange ikiwa unatimiza masharti ya mipango hii. Hali maalum za masharti haya zinaweza kuidhinishwa na uongozi mkuu kwa nia njema kulingana na hali. “Nia njema” itategemea ukweli na hali, na inaweza kujumuisha:
    - Waliokosa kipindi cha kujiandikisha cha kila mwaka na hawapatikani katika aina ya tukio la kubadilisha maisha nje ya kipindi cha kujiandikisha cha kila mwaka.
    - Wale ambao watalemewa na mzigo wa kifedha kwa mgonjwa kujiandikisha katika mpango wa afya ulioidhinishwa kuliko kutojiandikisha.

## B. Njia Ambayo Wagonjwa Wanaweza Kutuma Maombi ya Msaada wa Fedha

Ikiwa hakuna mawasiliano yoyote kutoka mgonjwa kuhusu msaada wa fedha, au mgonjwa hawezi kujaza utaratibu wa kutuma maombi unaohitajika chini ya Sera hii, bado wagonjwa kama hao wanaweza kuzingatiwa kwenye ustahiki wa msaada wa fedha kwa msingi wa makisio.

1. D-HH itatafuta vyanzo vingine vya bima na/au malipo kutoka kwenye serikali kuu, jimbo au mipango mingine na kusaidia wagonjwa kutuma maombi ya kupokea mipango kama hiyo. Kuhusiana na madeni yoyote yaliyobaki baada ya fedha za vyanzo kama hivyo kutumika, D-HH itafanya utathmini wa kibinafsi wa mahitaji ya kifedha ya mgonjwa ili kubainisha ikiwa mtu anatimiza masharti ya kupokea msaada chini ya sera hii, kwa kutumia utaratibu ufuatao:
    - Mgonjwa au mdhamini anatakiwa kutuma maombi kwenye fomu iliyoidhinishwa na usimamizi wa D-HH na atoe hati na maelezo kama hayo ya kibinafsi, ya kifedha na hati na maelezo mengine yanayohitajika ili D-HH iweze kubainisha ikiwa mtu huyo anatimiza masharti ya kupokea msaada, ikiwa ni pamoja na, lakini si tu, hati za kuthibitisha Mapato ya Familia na mali zilizopo au rasilimali zingine. Ikiwa D-HH haitapokea maombi au hati nyingine yoyote ya ziada inayohitajika kutoka kwa mgonjwa au mdhamini wa mgonjwa, D-HH inaweza kuamua iwapo mgonjwa anatimiza masharti ya kupokea msaada wa fedha kwa msingi wa kukisia.

- Badala ya kutumia maombi na hati za ziada kutoka kwa mgonjwa, mfanyakazi anaweza kutumia njia yoyote kati ya zifuatazo ili kuthibitisha mapendekezo ya kuidhinishwa kwa maombi ya msaada wa fedha:
- D-HH inaweza kutumia mtoa huduma mmoja au zaidi kutathmini watu iwapo wanatimiza masharti kwa kutumia vyanzo vya data vinavyopatikana hadharani ambavyo vinatoa maelezo kuhusu tabia na uwezo wa kulipa wa mgonjwa au mdhamini.
- Hali ya sasa ya kutimiza masharti ya bima ya Medicaid.
- Taarifa ya sasa kutoka kwenye mamlaka ya masuala ya nyumba ya Kitaifa au Jimbo.
- Uthibitisho kutoka kwenye makao ya wasio na nyumba au Kituo cha Afya Kilichoidhinishwa na Serikali.
- Hati ya kuthibitisha kufungwa gerezani bila chanzo cha malipo kutoka kwenye kituo cha kurekebisha tabia.
- Kwa mgonjwa binafsi, thibitisho la matamshi ya mgonjwa la mapato na mali, badala ya hati ya kuthibitisha, linaweza kukubaliwa kwa kutegemea akaunti moja (1) pekee, muradi salio lililo kwenye kaunti hiyo ni chini ya $1,000.

2. Inapendekezwa, lakini si lazima, kwamba maombi ya msaada wa fedha na ubainishaji wa mahitaji ya kifedha vinahitaji kufanywa kabla ya kutoa huduma za matibabu yasiyo ya dharura. Hata hivyo, mgonjwa anaweza kuzingatiwa kupewa msaada wa fedha wakati wowote katika kipindi cha ukusanyaji wa madeni. Maombi yaliyoidhinishwa ya msaada wa fedha yanatumika kwa madeni yote ambayo mgonjwa ametuma maombi ya kupata ufadhili wake, pamoja na huduma za matibabu ya dharura na huduma zingine muhimu za matibabu alizopokea kwa kipindi cha muda, tarehe za huduma kabla ya kupokewa kwa maombi ya msaada wa fedha, ikijumuisha madeni yaliyoripotiwa katika shirika la ukusanyaji wa madeni na huduma zozote zilizotolewa kabla au katika tarehe ya mwisho wa matumizi iliyoandikwa kwenye barua ya uthibitishaji muradi huduma haijatiwa chini yake. Baada ya muda huo au wakati wowote ambapo maelezo ya ziada yanayohusiana na hali ya kutimiza masharti ya mgonjwa yatakapopatikana, D-HH itathmini upya mahitaji ya kifedha ya mgonjwa kwa mujibu wa Sera hii.

   D-H H inatambua maamuzi yaliyofanywa na mipango ifuatayo ya kutoa msaada bila kuomba nakala za maombi. D-HH ina haki ya kukubali au kukataa maamuzi yaliyofanywa nje ya mwongozo wa D- HH yaliyofanywa na mashirika yaliyoorodheshwa hapa chini. Malipo yote yanayostahili kulipwa na mgonjwa mwenyewe au pesa zozote zinazostahili kulipwa na mgonjwa zinapaswa kuombwa kwa mujibu wa masharti ya mipango hiyo.

   - NH Health Access Network Card kwa wagonjwa wenye bima pekee
   - Good Neighbor Health Clinic
   - Manchester Community Health Center
   - Nashua Area Health Clinic
   - Mobile Community Health
   - Teen Health Clinic
   - Hali ya sasa ya kutimiza masharti ya bima ya Medicaid ikiwa haiendelei kutumika kushughulikia huduma za awali
   - Mgonjwa aliyeaga dunia asiye na mali (kama ilivyothibitishwa na mtekelezaji au jimbo)

3. Ni lengo la D-HH kushughulikia maombi ya msaada wa fedha na kufahamisha

mgonjwa kuhusu uamuzi uliotolewa ndani ya siku 30 baada ya kupokea maombi yaliyotumwa.

4. **Mchakato wa Kukata Rufaa**: Ikiwa D-HH itakataa kutoa sehemu ya msaada au msaada wote wa fedha, mgonjwa (au ajenti wake) anaweza kukata rufaa kuhusu uamuzi huo ndani ya siku 30. Lazima mgonjwa aandike barua kwa Director of Eligibility and Enrollment ili kufafanua kwa nini uamuzi uliofanywa na D-HH haufai. Barua ya rufaa itakaguliwa na D-HH na mgonjwa atafahamishwa kuhusu uamuzi wa mwisho ndani ya siku 30 baada ya ombi la rufaa kupokewa.

## C. Ubainishaji wa Kiasi cha Fedha za Msaada

Malipo yote ya bima na mabadiliko ya mkataba pamoja na punguzo la gharama za huduma zisizoshughulikiwa na bima huzingatiwa katika marekebisho ya kiasi cha fedha za msaada zinazoombwa. Soma Sera ya Punguzo la Gharama za Huduma za Mgonjwa Asiye na Bima ya D-HH: Kitengo cha Kusimamia Ushuru (kiungo kilicho hapa chini)

Ikiwa mtu ameidhinishwa kupokea msaada wa fedha, kiasi cha pesa za msaada huo za kutolewa kwa ajili ya matibabu yanayoruhusiwa itakuwa kama ifuatavyo:

- Mapato ya familia yanayolingana na/au ya chini ya 225% ya FPL yatapokea msaada wa fedha wa 100%
- Mapato ya familia ya kati ya 226% - 250% ya FPL yatapokea punguzo la 75%
- Mapato ya familia ya kati ya 251% - 275% ya FPL yatapokea punguzo la 50%
- Mapato ya familia ya kati ya 276% - 300% ya FPL yatapokea punguzo la 25%.
- Kama ilivyobainishwa hapo juu, wagonjwa ambao mapato yao ya familia yanazidi 300% ya FPL wanaweza kustahiki kupokea punguzo kulingana na deni wanalopaswa kulipa wenyewe. Mapunguzo yatatolewa ili jumla ya bili ya kulipa mwenyewe isizidi 10% ya mapato ya jumla ya miaka 2, pamoja na 10% ya mali inayozidi thamani ya mali zinazolindwa na bima zilizobainishwa mapema kwenye Sera. Mapunguzo yoyote kando na yaliyobainishwa hapo juu, lazima yaidhinishwe na Financial Assistance Appeals Committee kulingana na rufaa iliyoandikwa na mgonjwa au mtu anayehusika.
- Wagonjwa wanaotimiza vigezo vya kupokea Msaada wa Fedha kwa Msingi wa Makisio, watapokea msaada wa fedha wa 100%.

Wagonjwa wasio na bima, ikijumuisha wagonjwa wasio na bima wanaotimiza masharti ya kupokea msaada wa fedha chini ya Sera hii, huenda wasitozwe kiasi chochote kinachozidi kiasi cha kawaida ambacho hutozwa wagonjwa walio na bima inayoshughulikia matibabu kama hayo. Dartmouth-Hitchcock hutoa punguzo kwa gharama za jumla kwa madeni yote ya wagonjwa wasio na bima, hatua ambayo hupunguza kiasi cha deni ambalo mgonjwa anatarajiwa kulipa.

Punguzo hutolewa kulingana na mbinu ya "ada ya huduma ya Medicare ya kipindi cha nyuma pamoja na walipaji wa kibinafsi" kama ilivyobainishwa chini ya kanuni zinazotumika za utekelezaji wa Kifungu cha 501(r) cha Kanuni ya Mapato ya Ndani. Punguzo hili huwekwa kabla ya kutoza mgonjwa na kabla ya kuweka marekebisho yoyote ya msaada wa fedha. Punguzo hili halitumiki kwenye kiasi chochote cha malipo yanayoshirikiwa, malipo ya bima yanayoshirikiwa, malipo ya lazima, malipo

ya mapema au malipo ya huduma za ziada ambayo tayari yanaonyesha punguzo lolote linalohitajika, au kwenye huduma zilizoainishwa kama huduma zisizoshughulikiwa na bima na kampuni zote za bima.

Kwa mwaka wa fedha wa kuanzia tarehe 1/7/2021 - 30/6/2022, viwango vifuatavyo vya punguzo vinatumika:

| | |
|---|---|
| Dartmouth-Hitchcock Clinic | 61.6% |
| Mary Hitchcock Memorial Hospital | 61.6% |
| Cheshire Medical Center | 64.3% |
| Alice Peck Day Memorial Hospital | 30.8% |
| New London Hospital | 51.7% |

## D. Mawasiliano Kuhusu Sera ya Msaada wa Fedha ya D-HH kwa Wagonjwa na katika Jamii

- Uelekezaji wa wagonjwa ili wapokee msaada wa fedha unaweza kufanywa na ajenti au mfanyakazi yeyote wa D-HH, ikiwa ni pamoja na madaktari, wauguzi, washauri wa fedha, watoa huduma za jamii, wasimamizi wa hali, makasisi na wafadhili wa kidini. Maombi ya msaada wa fedha yanaweza kutumwa na mgonjwa au mwanafamilia, rafiki wa karibu au ajenti wa mgonjwa, kwa kutegemea sheria za faragha zinazotumika.

- Maelezo kuhusu msaada wa fedha kutoka D-HH, ikiwa ni pamoja na, wala si tu, sera hii, muhtasari wa lugha rahisi ya sera hii, fomu ya kutuma maombi na maelezo kuhusu utaratibu na sera za ukusanyaji wa madeni ya wagonjwa za D-HH, yatatolewa kwa umma na kwa wagonjwa wa D-HH kupitia angalau mbinu zilizobainishwa hapa chini:
  - Kwenye tovuti za D-HH
  - Yatachapishwa katika maeneo ya kutoa huduma kwa wagonjwa,
  - Yatapatikana kwenye Kadi za Maelezo katika idara za usajili na uandikishaji,
  - Yatapatikana katika maeneo mengine ya umma kama itakavyobainishwa na D-HH
  - Kutolewa katika lugha za msingi zinazozungumzwa na watu wanaohudumiwa na D-H/CMC; huduma za tafsiri zitatumika panapohitajika.

- Ikiwa deni litaidhinishwa, mgonjwa atatumiwa barua inayoonyesha kuidhinishwa.

## E. Usaidizi wa Kujaza Fomu za Maombi

Unaweza kupokea usaidizi wa ana kwa ana wa kujaza fomu hii ya maombi katika maeneo yafuatayo:

| | | |
|---|---|---|
| **Dartmouth-Hitchcock**<br>Hifadhi Moja ya Kituo cha Matibabu<br>Lebanon, NH 03756<br>(603) 650-8051 | **Dartmouth-Hitchcock Clinic Concord**<br>253 Pleasant Street<br>Concord, NH 03301<br>(603) 229-5080 | **Dartmouth-Hitchcock Clinic Manchester**<br>100 Hitchcock Way<br>Manchester, NH 03104<br>(603) 695-2692 |
| **Dartmouth-Hitchcock Nashua**<br>2300 Southwood Drive<br>Nashua, NH 03063<br>(603) 577-4055 | **Dartmouth-Hitchcock Keene**<br>580-590 Court Street<br>Keene, NH 03431<br>(603) 354-5454 kiendelezi:4444 | **Cheshire Medical Center**<br>580 Court Street<br>Keene, NH 03431<br>(603) 354-5430 |

| Alice Peck Day Memorial Hospital<br>10 Alice Peck Day Drive<br>Lebanon, NH 03766<br>(603) 443-9579 | New London Hospital<br>273 County Road<br>New London, NH 03257<br>(603)526-2911 | |
|---|---|---|

Utaendelea kulipia huduma zozote unazopokea hadi ombi ulilotuma litakapopokewa.

Njia za ziada zinaweza kupatikana kupitia New Hampshire Health Access Network (https://www.healthynh.com/nh-health-access-network.html)

## F. Mchakato wa Kukata Rufaa ya Msaada wa Fedha

- Ikiwa deni halitaidhinishwa, mgonjwa atatumiwa barua ya kukataliwa kwa deni au nakala ya maombi inayoonyesha sababu ya kukataliwa, ikiwa ataomba. Barua inayobainisha mchakato rasmi wa kukata rufaa itatumwa pia kwa kila ombi litakalokataliwa au barua zinazotoa sehemu ya punguzo pekee.
- Kamati ya Viongozi watatu wa D-HH ambao hawahusiki katika mchakato halisi watakagua rufaa na kutoa mapendekezo kuhusu rufaa zote za kukataliwa kwa maombi.

## G. Kutimiza Masharti ya Msaada wa Fedha wa Muda

D-H H inaweza kutumia watu wengine kukagua maelezo ya mgonjwa ili kutathmini mahitaji yake ya fedha. Ukaguzi huu hutumia muundo wa ubashiriki unaotambulika na sekta ya huduma ya afya ambao unatokana na hifadhidata za rekodi za umma. Muundo huu hutumia rekodi ya data ya umma ili kutathmini kiwango cha uwezo wa kifedha na uchumi wa jamii ambayo inajumuisha makadirio ya mapato, rasilimali na uwezo wa kupata pesa. Kikundi cha kanuni za muundo kimebuniwa ili kutathmini kila mgonjwa kwa kutumia viwango sawa na hupimwa kulingana na kumbukumbu za kuidhinishwa kwa maombi ya msaada wa fedha ya mfumo wa Dartmouth-Hitchcock Health.

Maelezo kutoka kwenye muundo wa ubashiri yanaweza kutumiwa na D-HH kutoa ustahiki wa muda katika hali ambapo hakuna maelezo yaliyotolewa moja kwa moja na mgonjwa. Msaada wa fedha wa muda haupatikani kwa ajili ya kulipa madeni ambayo hayakushughulikiwa na bima ya Medicare.

Uchunguzi wa muda hutumiwa, bila kujali deni lililopo, kwenye akaunti zinazotimiza masharti zilizokaa kwa zaidi ya siku 120 baada ya kutolewa kwa taarifa, baada ya kutolewa kwa notisi za kukusanya deni na kabla ya akaunti kuelekezwa kwa shirika la nje la ukusanyaji wa madeni ili kutoa msaada wa fedha kwa wagonjwa ambao hawajakuwa wakijibu mawasiliano ya taarifa za chaguo la kujaza Fomu ya Maombi ya Msaada wa Fedha. Akaunti za kurithisha mali za walioaga dunia ambazo zimepitisha vikomo vya muda zinatimiza masharti ya uchunguzi kwa misingi ya kukisia.

Ufadhili wa Muda hauchukui nafasi ya michakato ya kawaida ya FAP; hutumiwa kutoa mchango wa ziada katika juhudi hizi na unalenga wagonjwa ambao vinginevyo hawajibu mawasiliano ya mchakato wa kawaida wa FAP. Katika juhudi za kuondoa vizuizi kwa wagonjwa hawa na kuboresha manufaa tunayowapa wagonjwa, hospitali hutumia mchakato wa uchunguzi wa mtandaoni kabla ya kuwekwa kwenye orodha ya akaunti za madeni yasiyoweza kulipwa. Wagonjwa wanaotimiza masharti ya ufadhili kwa misingi ya kukisia hawataripotiwa kwa shirika la ukusanyaji wa madeni.

Mchakato wa kujumuishwa katika mpango unalingana na algoriti za kutoa alama kwa kutumia maelezo ya rekodi ya umma na kwa kawaida hautumii kipimo cha ada zinazobadilika. Mapunguzo yasiyo kamili hayaruhusiwi na Ufadhili kwa Misingi ya Kukisia. Watu mahususi wanaokusudiwa ni pamoja na:

- Walioaga dunia wasio na mali au familia isiyojulikana
- Watu wasio na makao ya kudumu
- Watu waliotenganishwa na familia wasiopokea msaada wowote
- Wagonjwa ambao hawajibu mawasiliano au wasioweza kukamilisha mchakato wa kawaida

Mchakato wa kutoa alama za kupokea ufadhili wa muda hutumia kigezo cha uchumi wa jamii na data isiyotokana na mikopo. Mchakato wa uchunguzi hutumia hifadhidata ya umma yenye maelezo yafuatayo:

- Shughuli za Mtumiaji
- Rekodi za Mahakama
- Umiliki wa Mali
- Umiliki wa nyumba dhidi ya mkodishaji
- Data ya takwimu za watu, uchumi wa eneo
- Hali ya ajira
- Faili za Huduma za Umma
- Faili za
- Serikali (Hali ya kufilisika, SSN, watu walioaga dunia)

Ufadhili wa muda hautegemei data ya ripoti ya ofisi ya mikopo na huondoa maombi ya kuangalia alama ya mikopo kwenye ripoti ya mkopo. Maelezo yaliyopatikana hujumuisha alama ya Ufadhili kwa Msingi wa kukisia ya 0 (anayeihitaji zaidi) hadi 1000 (asiyehitaji sana). Maelezo hayo hubashiri mahitaji ya kuwa na mdhamini kulingana na vigezo vinavyojulikana ikiwa ni pamoja na, wala si tu Mapato, Mali na Uwezo wa kupata pesa.

Kurejeshewa pesa:

Ikiwa mgonjwa amelipa deni linalostahili kulipwa na kisha atume Maombi ya Msaada wa Fedha ambayo yataidhinishwa kwa msaada wa fedha kupitia mchakato wa kutuma maombi, hospitali itarejesha kiasi chochote cha pesa ambazo mgonjwa amelipa kwa ajili ya matibabu.

## H. Viwango vya Ubainishaji wa Ufadhili

- Viwango vya uidhinishaji ni kama vifuatavyo:

| Cheo | Dartmouth-Hitchcock | Hospitali Wanachama |
|---|---|---|
| Makamu wa Rais/ CFO/Rais | Zaidi ya $350,000 | Zaidi ya $100,000 |
| Mkurugenzi Usimamizi wa Mapato | Zaidi ya $50,0000 | Zaidi ya $50,0000 |
| Mkurugenzi – Conifer | Hadi $50,000 | Hadi $50,000 |
| Meneja – Conifer | Hadi $5000 | Hadi $5000 |
| Msimamizi – Conifer | Hadi $1000 | Hadi $1000 |
| Mwakilishi wa Akaunti – Conifer | Hadi $500 | Hadi $500 |

## I. Huduma Zisizojumuishwa kwenye Msaada wa Fedha – Huduma

### a. Hali Maalum

- Taratibu za matibabu zilizo hapa chini hazikusudiwi kuwa orodha kamili ya huduma.
- Huduma za matibabu zisizo muhimu, kama inavyobainishwa na Mtoa Huduma zinaweza kutojumuishwa.
- Juhudi zote zitafanywa ili kumfahamisha mgonjwa kabla ya kupokea huduma ya matibabu yoyote mapya yasiyoshughulikiwa chini ya Mpango wa Msaada wa Fedha.

### b. Upasuaji wa Urembo Usio wa Lazima (haushughulikiwi)

- Upasuaji wa Kuondoa Kapsuli na Matiti Yaliyopandikizwa na viungo vya kupandikizwa
- Upasuaji wa kuimarisha matiti (Kupandisha matiti juu)
- Upasuaji wa Kuondoa Matiti ya Wanaume (Uondoaji wa Matiti ya Wanaume)
- Upasuaji wa Kuondoa Matiti (Urembo)
- Upasuaji wa Kuondoa Mikunjo ya Uso (Kuboresha Uso)
- Upasuaji wa Kukarabati Vigubiko vya Macho (Vigubiko vya Macho)
- Upasuaji wa Kupandisha Juu Nyusi (mafuta/mikunjo kwenye paji la uso)
- Upasuaji wa Kuongeza Ukubwa wa Matiti (upandikizaji wa matiti)
- Upasuaji wa Kupunguza Ukubwa wa Matiti (upasuaji wa kupunguza ukubwa wa matiti haushughulikiwi na bima)
- Upasuaji wa Kubadilisha Umbo la Pua (pua)
- Upasuaji wa Matibabu ya Ngozi
- Upasuaji wa Kupunguza Ukubwa wa Tumbo (kupunguza ukubwa wa tumbo)
- Upasuaji wa aina yoyote wa kuondoa mafuta ya ziada mwilini (liposuction) – unaweza pia kuorodheshwa kama uondoaji wa mafuta au ngozi ya ziada, ambao hauzingatiwi kama huduma muhimu ya matibabu

  **Kidokezo:** Matibabu ya upasuaji ya hapo juu kwa kawaida huchunguzwa na kubainishwa na Waratibu wa Maelezo ya Fedha

### c. Uhimilishaji Kibandia

- Upasuaji wa Kufunga Mishipa ya Uzazi ya Mwanamke (kukata au kuziba mishipa ya uzazi ya mwanamke)
- Upasuaji wa Kuzibua Mishipa ya Uzazi ya Mwanaume (kufungua upya mishipa ya uzazi ya mwanaume)
- Upasuaji wa tumbo au fupanyonga kwa matibabu ya utasa (Mipango ya IUI - IVF - GIFT)
- Matibabu ya utasa

### d. Mengine

- Tiba vitobo
- Huduma za Matibabu ya Maungo
- Vifaa vya kusaidia kusikia na ukarabati
- Miwani
- Tiba ya kukanda mwili
- Dawa za maagizo ya daktari na dawa za kununuliwa dukani

- Kliniki ya Tiba ya Usafiri
- Utafiti wa Damu ya Kiungamwana
- Mauzo ya Rejareja
- Huduma zinazotolewa na Renaissance Psychiatry of New England, LLC

**e. Msaada wa Fedha hutolewa TU baada ya Hitaji la Matibabu kuidhinishwa**

- Upasuaji wa Unene Kupita Kiasi

**f. Maeneo ya Manchester and Nashua Pekee**

- **Uchunguzi wa Kawaida wa Macho**
    - Hushughulikiwa na bima tu ikiwa umebainishwa kuwa ni huduma muhimu ya matibabu na/au kuna ugonjwa wa msingi.
    - Katika hali ambapo magonjwa haya HAYAPO, mratibu atamfahamisha mgonjwa kuwa msaada wa fedha hautatolewa.
    - Opthamolojia ya Keene na Lebanon inapuuza huduma hizi.

**g. Hali maalum**

- Baadhi ya huduma zinazopatikana chini ya aina ya huduma za ziada na huduma za matibabu yasiyo muhimu, zinaweza kushughulikiwa chini ya Sera ya Msaada wa Fedha ya D-HH kwenye baadhi ya huduma au huduma zote zinazohusiana na kipindi cha matibabu.
- Sera na taratibu zitabainishwa kwenye huduma zinazojulikana na kuhifadhiwa na Timu ya Patient Access Resource.
- Hizi zitakaguliwa kila mwaka ili kufanyiwa marekebisho muhimu.
- Hali mahususi zitakaguliwa na viongozi wa Patient Access na Naibu Rais wa Usimamizi wa Mapato ili kuidhinishwa kwa hali maalum.

**h. Huduma Zisizojumuishwa kwenye Msaada wa Fedha – Watoa Huduma Wasio wa D-H**

- Cheshire – Radiology Associates of Keene
- Cheshire – Surgicare Medical Equipment
- Cheshire – Monadnock Family Services
- Manchester – Foundation Medical Partners
- Manchester – Amoskeag Anesthesia
- Manchester – Dietician Services
- Manchester – Alliance Health Services/Catholic Medical Center
- Bedford – Alliance Health Services/Catholic Medical Center
- Nashua – Greater Nashua Mental Health Center (Mtoa Huduma za Jamii)
- Nashua – Nashua Anesthesiologist Group
- Nashua – St. Joseph's Hospital (PT/Huduma za Kurekebisha Tabia)
- Concord – Riverbend Community Mental Health
- Concord – Services provided Concord Hospital
- Lebanon – Orthocare medical equipment
- Alice Peck Day – Medstream Anesthesia
- Alice Peck Day – Upper Valley Neurology and Neurosurgery (UVNN)
- Alice Peck Day – Envision (ED & Hospitalist)*
- New London Hospital – Concord Orthopaedics (huduma za kitaalamu)
- New London Hospital – Concord Podiatry (huduma za kitaalamu)
- New London Hospital – Concord Urology (huduma za kitaalamu)

- New London Hospital – Counseling Associates (huduma za kitaalamu)
- New London Hospital – Dr. Richard Rosata – Oral and Maxillofacial Surgery (huduma za kitaalamu)
- New London Hospital – Valley Regional Healthcare (huduma za kitaalamu)
- New London Hospital – Peraza Dermatology Group (huduma za kitaalamu)
- New London Hospital – Optical Shop
- New London Hospital – Midwife Services (huduma za kitaalamu)

*Mkataba Umekomeshwa

## V. Marejeleo HAMNA

| **Mmiliki Anayewajibika:** | Finance Division Corporate | **Watu wa kuwasiliana nao:** | Kimberly Mender |
|---|---|---|---|
| **Imeidhinishwa Na:** | Afisa Mkuu - Fedha; Kamati Inayoshughulikia Sera (COPS); Ofisi Inayoshughulikia Sera - Sera za Shirika Pekee; Gross, Daniel; Kays, Kieran; Naimie, Tina; Roberts, Todd | **Toleo la #** | 11 |
| **Tarehe ya Sasa ya Kuidhinishwa:** | 11/08/2021 | **Kitambulisho cha Hati ya Zamani:** | RMD.0031 |
| **Tarehe ya Sera Kuanza Kutumika:** | 11/08/2021<br>Imeidhinishwa na MHMH/DHC Kamati ya Fedha 23/6/2016; MHMH/DHC Bodi za Wadhamini 24/6/16 | | |
| **Sera na Taratibu Husika:** | Sera ya Punguzo la Gharama za Huduma za Wagonjwa Wasio na Bima - Kitengo cha Kusimamia UshuruSera ya Mikopo na Ukusanyaji<br>Sera ya Malipo ya Bajeti - Kitengo cha Usimamizi wa Mapato | | |
| **Zana za Usaidizi wa Kazi Husika:** | | | |